JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MJI WA MAKAMBAKO
SHULE YA SEKONDARI KIPAGAMO

S.L.P 110,

MAKAMBAKO.

KUMB NA. KIPSS/ADM/VOL.1/……

JINA LA MWANAFUNZI

…….

Ndugu,

YAH: <u>MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE KWA MWANAFUNZI WA KIDATO CHA KWANZA (I) MWAKA 2021</u>

Napenda kuchukua nafasi hii kukupongeza kwa kuchaguliwa kuingia kidato cha kwanza katika shule ya sekondari **KIPAGAMO**. Shule itafunguliwa tarehe **11/01/2021** siku ya Jumatatu saa 1:00 asubuhi.**Kila mwanafunzi wa kidato cha kwanza afike siku hiyo tayari kwa masomo**. Nafasi uliyopewa inatamaniwa na wengi walioikosa. Hivyo, huna budi kuijali na kuitumia kwa manufaa ya taifa.

Utakuwa na wajibu wa kusoma kwa bidii, kutii na kufuata sheria za shule, kushiriki kikamilifu katika kazi za mikono, uzalishaji mali, kuishi kwa amani, upendo na ushirikiano na watumishi pamoja na wanafunzi wenzako ili kupata elimu bora kwa maisha endelevu.

MAELEZO KUHUSU SHULE

Shule ya sekondari **KIPAGAMO** ni shule ya kutwa na ni ya mchanganyiko. Ipo umbali wa kilometa tatu na nusu ($3^1/_2$) kutoka njia panda au makutano ya barabara kuu ya Songea na Mbeya kuelekea Iringa.

UNAKARIBISHWA SANA

……
R.A. SANDAGILA
MKUU WA SHULE
0755776368

MAELEKEZO MUHIMU:

Maelekezo haya yanahusu Sare, Nguo na vifaa vya michezo, vifaa vya darasani na vifaa vya usafi.

NA	WAVULANA	IDADI/ JOZI	WASICHANA	IDADI/JOZI
1	***SARE YA SHULE***			
	➢ Suruali rangi ya **DARK BLUE** (iwe na mifuko mitatu tu, isiwe ya kubana na iwe na 'turn up' au marinda. ➢ Mashati meupe ya mikono mifupi ➢ Viatu vyeusi vya ngozi (vyenye visigino vifupi na vyenye kamba) ➢ Soksi nyeusi ➢ Sweta (rangi ya uzi imeambatanishwa)	02 02 02 02 02	➢ Suruali rangi ya **DARK BLUE** (isiyo ya kubana) ➢ Blauzi nyeupe mikono mirefu ➢ Viatu vyeusi vya ngozi (vyenye visigino vifupi na vyenye kamba) ➢ Soksi nyeupe ➢ Sweta (rangi ya uzi imeambatanishwa)	02 02 02 02 02
2	***NGUO ZA MICHEZO NA VIFAA VYA MICHEZO***			
	❖ Raba nyeusi ❖ Fulana (dark bluu) ❖ Bukta ❖ Traki suti (dark blue)	01 01 01 01	❖ Raba nyeusi ❖ Fulana (nyeupe) ❖ Bukta ❖ Traki suti (dark blue)	01 01 01 01
3	***VIFAA VYA DARASANI***			
	✓ Madaftari mapya ▪ Makubwa (counter book Q3) ▪ Madogo/kawaida ✓ Mkebe wa vifaa vya hisabati (mathematical set) ✓ Rula futi moja ✓ Kalamu ya wino wa bluu au mweusi ✓ Kalamu ya risasi (penseli) ✓ Mkoba nadhifu wa kubebea daftari (**begi**) na siyo mfuko. ✓ Jalada (spring file) ✓ Oxford English Dictionary	 10 04 01 01 02 02 01 01 01	✓ Madaftari mapya ▪ Makubwa (counter book Q3) ▪ Madogo/kawaida ✓ Mkebe wa vifaa vya hisabati (mathematical set) ✓ Rula futi moja ✓ Kalamu ya wino wa bluu au mweusi ✓ Kalamu ya risasi (penseli) ✓ Mkoba nadhifu wa kubebea daftari (**begi**) na siyo mfuko. ✓ Jalada (spring file) ✓ Oxford English Dictionary	 10 04 01 01 02 02 01 01 01
4	***VIFAA VINGINE***			
	▪ bunda la karatasi (rimu) ▪ ufagio ▪ jembe	01 01 01	▪ bunda la karatasi (rimu) ▪ Ufagio ▪ Ndoo lita 10	01 01 01

KUMBUKA:

*i. Rangi ya **Hijabu** kwa wanafunzi wa **Dini ya Kiislamu** iwe **nyeupe**.*

*ii. Katika ushonaji wa **sare** za shule wanafunzi wa kike wazingatie **mchoro** ulioambatanishwa na fomu hii.*

MCHANGO WA CHAKULA

Kwa kuzingatia maagizo ya serikali na umuhimu wa wanafunzi kupata chakula cha mchana shuleni michango ya chakula itakuwa kama ifuatavyo:

Na	AINA YA CHAKULA/FEDHA	IDADI/KIASI	MAELEZO
1	Maharage safi ya aina moja	Kilo 20	Yaletwe kilo 10 kwa kila muhula
2	Mahindi safi	Kilo 40	Yaletwe kilo 20 kwa kila muhula
3	Fedha ya chakula	Tshs. 30,000/-	Zilipwe nusu kila muhula (yaani Tshs. 15,000/- kwa muhula)

Fedha ya chakula ni **Tshs. 30000/-** kiasi hiki cha fedha ni kwa mwaka mzima na ni kwa ajili ya kukoboa, kusaga, kulipa mpishi, kununua viungo, mafuta, vyombo vya kupikia na kuni. Kiasi hiki cha fedha ni kwa **mwaka mzima**. Inaweza kulipwa **Tshs. 15,000/-** kila muhula, na fedha hii ilipwe kupitia benki kwa akaunti namba **60301000018** tawi la **NMB Makambako**, jina la akaunti ni **KIPAGAMO SECONDARY SCHOOL** na risiti ya benki iletwe shuleni unapomleta mwanao kwa ajili ya usajili.

MUHIMU

Fomu zifuatazo ziwasilishwe shuleni siku ya kuripoti shule zikiwa zimejazwa kikamilifu:

i. Fomu ya kupima afya (Medical Examination Form)
ii. Fomu ya kukubali nafasi.
iii. Fomu ya maelezo binafsi.

Fomu hizi zimeambatanishwa na fomu hii ya maelekezo ya kujiunga na shule.

Mzazi/mlezi na **mwanafunzi** wasome sheria za shule na kuzielewa ikiwa ni pamoja na kukamilisha ujazaji wa fomu zilizoambatanishwa. Tunasisitiza **ujazaji sahihi** wa fomu ya kupima afya (na kwa wale wenye matatizo ya kiafya walete fomu na vyeti husika). Hii itasaidia kutoa msaada sahihi pindi wapatapo matatizo.

Pia fika shuleni pamoja na barua hii.

SHULE ITAFUNGULIWA TAREHE 11/01/2021, Saa 1:00 asubuhi siku ya Jumatatu; FIKA BILA KUKOSA TAYARI KWA KUANZA MASOMO.

Karibu sana Shule ya Sekondari Kipagamo

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA(OR-TAMISEMI)
HALMASHAURI YA MJI MAKAMBAKO.
SHULE YA SEKONDARI KIPAGAMO.

FOMU YA KUKUBALI NAFASI
A: MWANAFUNZI
JINA LA MWANAFUNZI……
ANUANI:……
TAREHE:…….

Mimi……..
nimekubali/sijakubali kujiunga na shule ya Sekondari Kipagamo.Nimesoma maagizo ya Shule kwa makini na kuyaelewa. Naahidi kuwa nitazingatia sheria/taaratibu za Shule kama nitakavyoelekezwa.

Sahihi ya
Mwanafunzi……..Tarehe……
……..

B:
MZAZI/MLEZI:……
……

JINA LA
MLEZI/MZAZI:……
……

ANUANI:……
……

TAREHE:……
……..

Mimi……
……

MZAZI/MLEZI
WA……
……...

Nimesoma kwa makini maagizo ya shule yaliyotolewa yanayomhusu mtoto wangu. Nimekubali/sijakubali kuwa mwanangu achukue nafasi hiyo. Naahidi pia kuwa nitashirikiana na uongozi wa shule katika kumkuza na kumlea mwanafunzi huyu kielimu na kitabia.

Sahii ya mzazi /mlezi …… Tarehe
…….

NB. FUTA ISIYOHUSIKA.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA(OR-TAMISEMI)
HALAMASHAURI YA MJI WA MAKAMBAKO
SHULE YA SEKONDARI KIPAGAMO.

MAELEKEZO BINAFSI YAMHUSUYO MWANAFUNZI

A . 1. Jina la mwanafunzi
……
2. mahali alipozaliwa wilaya …….. Mkoa ……
3.
Dini……Dhehebu……
……
B. 1. Baba mzima……Ndiyo/hapana
2. Mama mzima……Ndiyo/hapana
C. 1. Jina la mzazi /mlezi anayekutunza
……
2. Kazi ya
Mzazi/Mlezi……
……..
3. Anuani ya posta ya Mzazi/Mlezi
……..
4. Namba ya simu ya
Mzazi/Mlezi……
5. Mahali anapoishi
Mzazi/Mlezi(kijiji/mji)……(Wilaya)……Mkoa……
D. Majina na anuani za ndugu wengine wa karibu waohusika na malezi ya wanafunzi.
1. Jina
……Anuani/simu……
……
2. Jina
……Anuani/simu……
……
3.
Jina……Anuani/simu……
……..

E. Anuani ya Ofisi ya Katibu Kata Tawi/Kijiji ambapo Mzazi /Mlezi wa Mwanafunzi anaishi.

1.Kata ya ……
2.Anuani/simu……
Kijiji cha……..anuani/simu……

ZINGATIA :- Tafadhali ijaze fomu hii kwa uangalifu na kwa usafi wa hali ya juu.
Mwanafunzi anapaswa kuja na kopi ya cheti cha kuzaliwa(birth certificate).

PRESIDENT S OFFICE, REGINAL ADMINISTRATIVE AND LOCAL GOVERNMENTS.
MAKAMBAKO TOWN COUNCIL
KIPAGAMO SECONDARY SCHOOL.

P.O BOX 110,
MAKAMBAKO.
……

REF. NO KPSS/AD/2017/ ……
THE MEDICAL OFFICER,
……

REF; REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

Kindly examine (name); …… Age; ……
To determine her/his physical and mental fitness pursue.

1. Eye sight:_____
2. Hearing:_____
3. Speech:_____
4. Limbs:_____
5. Leprosy:_____
6. Epilepsy:_____
7. Cardiac disease:_____
8. Rheumatism:_____
9. Venereal:_____
10. Pregnancy(for girls):_____
11. Any other serious diseases:_____
12. Any disabilities:_____

Signature:_____
Designation:_____
Stamp:_____

Date:_____

SHERIA NA KANUNI ZA SHULE.

Sheria za shule zina lenga katika kumlea mwanafunzi awe na nidhamu, azingatie maadili ya taifa letu na hatimaye aishi kama raia mwema anayekubalika na jamii yetu. Ni imani yetu kuwa shule yenye wanafunzi wenye nidhamu hufanya vizuri katika taaluma.

HIVYO NI LAZIMA KWA KILA MWANFUNZI WA SHULE HII

1. Kuhudhulia masomo kila siku , tatizo la ugonjwa , msiba nk litaombewa ruhusa.
2. Kusalimu watu wote na hasa waliomzidi umri.
3. Kusimama mwalimu anapoingia darasani au wakati wa kuuliza na kujibu swali.
4. Kuwahi shuleni na kufanya usafi eneo alilopangiwa.
5. Kuvaa nguo za heshima ndefu shuleni na hata nyumbani.
6. Kutii sheria zote za shule.
7. Ni muhimu kutunza usafi wako binafsi na mazingira ya shule.
8. Kukaa kimya kwa nidhamu darasani.
9. Usizungumze na mwalimu au mtu aliyekuzidi umri ukiwa umekaa, mikono ikiwa mifukoni ama kofia kichwani au ukiwa umevaa miwani.
10. Mwanafunzi huruhusiwi kutembea usiku bila sababu yeyote hata kama atakuwa kwa wazazi wake.
11. Mwanafunzi kufanya sherehe usiku.
12. Mwanafunzi haruhusiwi kubishana na mwalimu au kiongozi yeyote uamuzi wa mwisho ni wa mwalimu. Malalamiko yeyote yapitie ngazi zilizowekwa kulingana na taratibu za shule.
13. Daima uwe msafi kimwili na mavazi. Uwe na nywele fupi, ndevu au masharubu haviruhusiwi shuleni.
14. Ni marufuku kwa mwanafunzi kujiunga na vilabu vya michezo nje ya shule.
15. Ni marufuku kwa mwanafunzi kushiriki katika vigenge vya usenganyaji au kusema uongo.
16. Usifanye biashara ya aina yeyote shuleni.
17. Usichelewe siku za kufungua shule au usiongeze siku za ruhusa.
18. Usikatae uteuzi wa wa kushiriki shughuli za michezo n.k
19. Usigune wakati mwalimu au kiongozi yeyote anapotoa tangazo kama kuna swali nyosha mikono,mkondo, mikondo ya ustaarabu ifuatwe.
20. Usibandike au kuandika tangazo lolote lile bila ruhusa ya mwalimu anayehusika.

NI MARUFUKU KWA WANAFUNZI:

(a) Kutumia lugha chafu kama matusi n.k
(b) Kutembelea nyumba za wageni au nyumba za walimu, baa, vilabu vya pombe na kumbi za starehe.
(c) Kufuga kucha, nywele, ndevu,kuvaa mikufu,kupaka marashi au rangi kucha au kuvaa hereni kuwa na kamera, radio, simu ya mkononi awapo shuleni.
(d) Kufanya mapenzi na wanafunzi wake au watu wengine wa nje.
(e) Kuambatana na makundi ya wahuni mitaani.
(f) Kuondoka shuleni kabla mda wa masomo kuisha (utoro)

MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANFUNZI AFUKUZWE SHULE MARA MOJA:

(a) Wizi
(b) Uasherati, ubakaji na ushoga.
(c) Ulevi wa aina yeyote, pombe au madawa ya kulevya.
(d) Uvutaji bangi.
(e) Makosa ya jinai.
(f) Kupigana au kupiga.
(g) Kuoa au kuolewa.
(h) Kupata mimba au kusababisha mimba ndani ya shule au nje ya shule.
(i) Kutoa mimba au kutumia vidongo au njia za uzazi wa mpango.
(j) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
(k) Kudharau bendera au wimbo wa Taifa.
(l) Kufanya, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au kuhatarisha amani ya shule wakati wowote.
(m) Kukataa kutii amri ya mkuu wa shule au mwalimu yeyote.

MAISHA YA SHULE NI MAZURI KWA WALE TU WATAKAOFUATA SHERIA ZA SHULE.